

MSURURU WA
KUBADILISHA, KUGEUZA
NA KUZUSHA

KUONDOSHA UTATA

KUHUSU MAANA YA HADITHI

**"NIMEAMRISHWA
KUPIGANA NA
WATU"**



KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU.

Kila jinsi ya sifa njema ni za Allah Mlezi wa ulimwengu. Rehema na amani zimshukie mtukufu wa manabii na mitume, Bwanetu na Nabii wetu Muhammad Mwaminifu, na Jamaa zake na Maswahaba zake wote.

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehema na amani zimshukie):

"Nimeamrishwa kupigana na watu hadi washuhudie kuwa hapana Mola anaestahiki kuabudiwa ispokuwa Allah na kuwa Muhammad ni mtume wa Allah, na wasimamishe swala, na watoe zaka. Basi wakifanya hilo wamehifadhika kutokana na mimi damu zao na mali yao ispokuwa kwa haki ya Uislamu, na hisabu yao ni kwa Allah aliyetukuka."¹

Maingilio ya Kufahamu Hadithi

Ili tufahamu maana ya hadithi kwa fahamu ilio sahihi inatakitana tuashirie pande mbili:

- Umuhimu wa lugha ya Kiarabu katika kufahamu nukuu.
- Kuusoma Uislamu kwa mtazamo mkamilifu.

Umukima wa Lugha ya Kiarabu Katika Kufahamu Nukuu

Hakika Mwenyezi Mungu ameitukuza lugha ya Kiarabu, akateremsha kitabu chake cha mwisho kwa lugha hio {Kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi} na akajaalia ndiyo lugha ya Mtume wa mwisho. Kwahio daraja ya lugha hii katika wahyi mbili (Qurani na Sunnah) ni maarufu na hapana shaka katika hilo...

Na kutojuwa lugha ya Kiarabu ni kutoijuwa dini na nukuu zake, haswa zile nukuu ambazo zina utata ambao hauondoki ispokuwa kwa kujua kanuni za lugha ya Kiarabu na misingi yake. Laa sivyo hakika kufahamu vibaya wakati wa kutekeleza hukmu zinazotoka kwa Allah na Mtume wake hupelekea kupatikane madhara na shari kubwa. Kwahio msingi wa kupotoka ni kufahamu vibaya yanatoka kwa Mungu na Mtume wake (rehema na amani zimshukie).

1- Muttafaqun ‘alayh. Imepokewa na Bukhari (25) (Kitabu cha Imani, Mlango wa ‘Lakini wakitubu, wakashika Sala, na wakatoa Zaka, basi waachilieni,’ na Muslim (22) (Kitabu cha Imani, Mlango wa Kuamrisha Kupigana na Watu Hadi Waseme Laa ilaaha illaLlah), kutokana na hadithi ya Abdullah bin Umar.

Mwenye kusoma nukuu za sheria (aya na hadithi), hana budi awe na mtazamo mkamilifu akusanye baina ya vitagaa (tandu) vyake na misingi yake, na maondoko yake na makusudio yake. Hana budi akusanye baina nukuu na yasiyobadilika katika dini, zile ambazo zitakua na undani na utata atazirudisha kwenye zilo wazi, kama ambavyo Quran imeeleza wazi, pamoja na kufahamu ujumla na umaalumu, na ilowachiliwa wazi na iliofungwa, na ambayo inahitaji kubainishwa na iliyobainishwa, na sababu ya kuteremshwa aya na sababu ya kupatikanwa hadithi, na mengineyo ambayo yanajulikana katika somo la Usul al-Fiqh. Ni lazima nukuu zisipuuzwe, kwani kufanya kazi ni bora kuliko kupuuza. Kwa kufanya hivi ndiyo kusudio litatufungukia wazi wazi. Kwani hakika ya haki hagawanyiki wala haipingani bali inatoka kwenye shubaka moja.

Swali: Kutokana na hadithi iliyo tajwa hapo mbeleni, je inafahamika kuhalalisha kumwaga damu na kuuwa kwa sababu ya itikadi?

Ili kujibu hili swali, kwanza tunasema:

Wenye kukosea katika kufahamu hadithi ni watu aina mbili.

Aina ya kwanza: ni vijana katika sisi ambao hawajasoma Uislamu kwa misingi yake na kanuni zake, na hata siku moja hawajawahi kuonja usamehevu wa mafunzo yake na misingi yake mikubwa ambayo yametilia umuhimu kufanya kuhifadhi nafsi ya mwanadamu --mwanadamu yeyote awe na itikadi yoyote-- ni lazima katika mambo ya lazima kwenye hii sheria samehevu na ni malengo ya msingi katika mambo matano yenye kuhifadhiwa katika sheria (Dini, nafsi, akili, cheo na mali). Allah amesema:

{Anayemuuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote.} [Al-Maidah:32]

Na Uislamu haukusimama katika mpaka wa kuihifadhi nafsi bali umeamrisha kuiheshimu wakati Qurani ilipotaja wazi msingi huu: {Na hakika tumewatukuza wanaadamu} [Al-Israa:70]. Na sunna ikaja na mfano wa kivitendo wa msingi huu bila kuzingatia tofauti ya kidini au itikadi. Na katika hilo ni pale Mtume (rehema na amani zimshukie) aliposimama sababu ya jeneza la Yahudi, na baada maswahaba waliposema kwa kushangaa kuwa ni jeneza la yahudi, akawajibu, "Kwani si nafsi?"²

2- Muttafaqun 'alayh. Imepokewa na Bukhari (1312), Kitabu cha Janaiz, Mlango wa Anaesimama Sababu ya Jeneza la Yahudi, na Muslim (961), Kitabu cha Jeneza, Mlango wa Kusimama Sababu ya Jeneza, kutokamana na hadithi ya Qays bin Sa'ad na Sahl bin Hunayf (radhi za Allah ziwashukie).

Lakini hawa hawajapokea kutoka kwa wanazuoni wanaostahiki ambao ni Wacha Mungu, ambao wameshuhudiwa kukubaliwa na kukita katika elimu. Ndipo ufahamu wao mbaya wa hadithi "Nimeamrishwa kupigana na watu..." ukawapelekea kuifanya hii hadithi ndiyo nguzo yao wanayoitumia kama dalili, na kuititia hii hadithi ndiyo kwa madai yao wanaitumia ili kubomoa, kuharibu na kulipua. Basi wakaeneza ujisadi kwenye ardhi kwa jina la dini, {Na Mwenyezi Mungu hawapendi waharibifu} [Al-Maidah:64]. Kwani ni damu ngapi zimemwagwa, na roho zilotolewa! Na hakika wamesababisha madhara kwao na kwa wengine na kwa umma wao, hadi wamekuwa ndiyo njia ya maadui kutekeleza mipango yao kwa namna wanayotambua na kwa namna wasiyotambua.

Na kipote kingine: kutokamana na ambao si waislamu, na waislamu ambao wameathirika na mafunzo yao, ambao wanauambatisha Uislamu na kila kasoro na matusi na wanaubandika kila tuhuma, wakidai kuwa ni dini ya kutishia na kuogopesha, na kuwa hajui kuishi vizuri na mwengine, na kuwa kwenye nukuu zake inabeba madai ya shari, kuuwa na kuharibu. Bali wamefikia kusema kuwa Uislamu haufai kwa maisha ya kisasa yenye amani na utulivu.

Na uhakika ni kuwa kile kipote cha kwanza cha vijana waliojhuriwa ndiyo sababu ya msingi ya kupatikana mtazamo huu wa dhulma katika akili za watu. Na hilo ni kwa sababu ya matendo yao maovu na kufanya mfumo wao kuwa ni ubepari na uharibifu, hadi ukawa Uislamu wote unahukumiwa kuititia matendo yao ambayo yanakosea na yanadhuru wala hayanufaishi.

*Nasi hatukukutuma ila
uwe ni Rehema kwa
walimwengu wote.*



KujiBu Fahamu Potofu

1- "Nimeamrishwa uqaatil (kupigana) na watu hadi washuhudie kuwa hapana Mola anaestahiki kuabudiwa ispokuwa Allah..."

Swali la kwanza: Je, katika hadithi kuna dalili ya kumuua mwingine, bali ulazima wake mpaka afuate dini ya Uislamu kama walivyofahamu kipote cha kwanza?

Swali la pili: Je, Uislamu ni dini ya kutishia na kuua, na nukuu zake zinajenga chuki na kutomkubali mwengine, kama namna walivyofahamu kipote cha pili?

KujiBu Fahamu Potofu

Hakika kuangalia kwa undani na makini wa ufahamu wa lugha katika matamshi ya hadithi inatuwekea wazi makusudio na inaondosha utata unaodhaniwa.

Maneno ya Kilugha: Tofauti Baina Napigana (Uqaati³) na Narwa (Aqtul)

Je, kunao tofauti baina ya 'uqaatil' na 'aqtul'?

Hili tamshi la undani ndilo mahali pa fahamu ya makosa katika akili zao. Utawaona wamechanganya baina ya 'uqatil' ambayo ndiyo iko kwenye hadithi na 'aqtul'. Baina ya haya maneno mawili kuna tofauti kubwa sana.

'Uqatil' (kupigana) ni katika matamshi ya kutendeana (mufa'ala) ambayo inamaanisha kushirikiana katika kitendo. Kwahio pande zote mbili zinapigana, kama unaposema 'tajadala', watesi wawili wamejadiliana katika mjadala, yaani kila mmoja katika wao amefanya mjadala. Na hapa kila mmoja wao amepigana vita.

Na hili ndilo lilimpelekea imamu mkubwa katika lugha nae ni Imam Shafi'i (Mungu amrehemu) aseme, "Neno 'al-qitaal' (kupigana) halitokamani na 'al-qatl' (kuuwa) kabisa."³

Na hili wamelinukuu wanazuoni wengi kama Ibn Daqiq Al-Id⁴, Ibn Rajab⁵, Ibn Hajar⁶ na wengineo hata Ibn Taymiyya⁷ mwenyewe pia...

3- Fath al-Baari (1/76)

4- Sharh Umadat al-Ahkam (2/220)

5- Jaami al-Ulum wal-Hikam cha ibn Rajab (uk. 230)

6- Fath al-Baari (1/76)

7- Majmu al-Fatawa (19/20), (28/354)

Swali: Je, muradi wa hadithi ni kuanuwa watu wote hadi waingie katika Uislamu?

Hapana na elfu hapana!... Hakuna hata mwanachuoni mmoja aliywahi kusema hivi katika karne zote zilopita. Bali inapingana na dini ya Uislamu yenyeye sheria nzuri. Na ili kubainisha hilo:

Ni kuwa tamshi la 'watu' ni katika jumla inayokusudiwa baadhi, na ina mifano mengi katika Qurani, Sunna na maneno ya Waarabu. Amesema Allah aliyetukuka:

{Na watangazie watu **Hija; watakujia kwa miguu**} [Al-Hajj:27]. Makusudio ya 'watu' hapa ni waumini peke yao na sio watu wote.

Na Allah mtukufu amesema: {Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utu uzima wake na atakuwa katika watu wema} [Aal Imran:46]. 'Watu' hapa ni waliozungumza na Maryam kuhusu mwanawewe na sio watu wote. Na Allah mtukufu amesema: {Walioambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutege-mewa} [Aal Imran:173]. Tamshi la kwanza la 'watu' anaekusudiwa ni Abu Sufyan, ndivyo alivyosema Mujahid na Ikrima.

Kwahio makusudio ya 'watu' hapa ni jumla inayokusudiwa maalumu nao ni washirikina waarabu ambao walimpiga vita Mtume (rehema na amani zimshukie), na walitaka kummaliza yeye na maswahaba zake, na kuimaliza Da'awa yake, na sio watu wote, na hakika imetajwa sifa yao katika Suratu Tawba: {Hawachungi kwa Muumini ujamaa wala ahadi; basi hao ndio warukao mipaka} [Tawbah:10]. Na: {Waliovunja viapo vyao na wakawa na hamu ya kumfukuza Mtume, nao ndio walio kuanzeni mara ya kwanza...} [Tawba:13]

Uhai wa Mtume

Maisha ambayo yanaipa nguvu rai tuloitaja ya wanazuoni wengi katika kuifahamu hadithi

Hakika mwenye kupeleleza katika maisha, mwenendo na matukio ya Mtume (rehema na amani zimshukie) atajuwa hakika kuwa yeye ni Rehema aliyetolewa kuwa zawadi kwa ulimwengu, na kuwa yeye ni mpole mwenye huruma kama Qurani ilivyomwita. Na hili halihitaji dalili, kwani yeye ni katika ambao historia imemuandika katika karatasi safi ambae uanadamu haujashuhudia mfano wake.

Kwani Mtume (rehema na amani zimshukie) alikuwa mwenye huruma hata kwa waliomfanya uadui kwanzia mwanzo wa jambo lake hadi mwisho wake. Na ikutoshe kuhusiana na hili:

8- Tafsiri ya At-Tabari (6/250-251)

9- Angalia: Hashiya ya As-Sindi kwa Sunan ya ibn Majah (2/457)

- Kukataa kwake (**rehema na amani zimshukie**) kuwaangamiza katika mwanzo wa ulinganizi wake na neno lake: "Ewe Mola, waongoze umma wangu. Hakika, wao hawajui." Alisema kwa uerevu wa utume na huruma ya ujumbe. Angalia kwa undani haya matamshi yake. Ameanza na dua, "Ewe Mola, waongoze..." Kisha akawanasibisha kwake pamoja na ukafiri wao, "umma wangu." Kisha akawatakia udhru, "Hakika, wao hawajui."
- Kuwasamehe kwake baada kuwa na uwezo juu yao, aliposema, "Nendeni. Hakikany ḡiyyi muko huru." Akawaachilia huru. Bali akasema kuzidisha kuhusiana na amani: "Anaeingia nyumba yake basi ana amani" na lau ingekuwa makusudio ni kuuwa basi angesema anaesilimu ndiye ana amani.

Mgongano Unaokataliwa

Vipi Mtume (rehema na amani zimshukie) aamrishe wasiokuwa waislamu wauliwe kisha aamrishe watendewe wema na wapewe zawadi?!

{Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanya wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.} [Mumtahana:8]

Imepokewa katika hadithi sahihi kuwa Umar (radhi za Allah zimshukie) aliona nguo nzuri ya hariri. Basi akasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, lau ungeinunua hii ili uivae siku ya Ijumaa na uwavalie wageni watapokujja." Akasema, "Ewe Umar, hakika si lingine anavaa hii ambae hana sehemu (akhera)." Kisha Mtume akapewa zawadi katika yale mapambo. Akampatia Umar zawadi. Umar akaja kwa Mtume (rehema na amani zimshukie) akamwambia, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, umeniletea hii na nimekusikia ukisema yale uliyoyasema." Akamwambia, "Hakika mimi sikukupatia ili uvae. Hakika nimekupatia ili uuze au uvuhe." Umar akampatia zawadi ndugu yake kwa mama ambae alikuwa mshirikina¹⁰, sababu yeye halazimiki na uharamu wa kuvaahariri kwa wanaume.

Na tukio hili lilikuwa katika zama za Madina katika mwaka wa ugeni (mwaka wa 8 baada ya Hijra), yaani baada ya Fat'hi Makka. Kwahio haifai kusema kuwa kuwaten-dea wema makafiri na uadilifu zilifutwa na aya ya upanga, kama walivyodai baadhi, kwani asiekuwa Muislamu akiwa ameishi kwa amani hafanyiwi uadui wala hapigwi vita. Bali anafaa kufanyiwi wema na kupewa zawadi.

10- Ameipokea Bukhari katika Al-Adab Al-Mufrad (71) (Mlango wa Kumuunga Jamaa Mshirikina).

Maelezo na Ufafanuzi ili Kuondosha Utata

Uislamu ni dini ya huruma na tabia njema. Nayo ni neema kubwa ambayo Mungu amewatendea wema wafuasi wake. Kwani Uislamu umekuja kuweka nidhamu ya mafungamano baina ya kiumbe na Muumba wake, na mafungamano ya Muislamu na Muislamu mwenzake, na mafungamano na ambae unataofautiana nae katika tikadi. Kwahio imekusanya pande zote za maisha, inatengeneza na inafaa katika kila wakati na kila sehemu. Na Muislamu anaihisi hii fadhila daima. Na akiwa mbali na umimi basi anataka aeneze heri hii kwa ubinadamu wote, mbali na kuwa ye ye ameamrishwa afikishe na alinganie kwa Allah kwa hekima na mawaidha mazuri, kulingania katika hali yake hio ni katika mambo ya lazima zaidi. Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Hakika akiongozwa mtu mmoja kwa ajili yako ni bora kwako kuliko ngamia wekundu."¹¹ Allah amesema: {Basi anayeongoka anaongoka kwa faida ya nafsi yake} [Yunus:108]. Na asiyekubali basi Allah amesema: {Hapana kulazimisha katika Dini. Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu} [al-Baqara:256]. Na Allah Mtukufu amemwambia Nabii wake mkarimu: {Angelitaka Mola wako Mlezi wangeliamini wote waliomo katika ardhi. Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?} [Yunus:99]

Kutokamana na muondoko huu ndipo Waislamu wamebeba jukumu la kulingania, na kufikisha mwangaza kwa watu wote, ili kupatikane kusuudika wanadamu duniani na akhera.

Lakini daima shari iko katika vita na kheri, na huo ndio mwendo wa maisha katika kila zama na sehemu.

Kwani baina ya kuwa Kulingania kwa Allah kwa vizuri kumesimama huenda kukaingiliwa. Bali ikabadilika kuingilia kwake kukawa ni kufanya uadui. Kwa ajili ya hio ndipo kupigana kunafaa kisheria, wakati Da'awa na watu wake watapofanyiwa uadui. Na kuilinda nafsi ni katika mambo ya lazima zaidi, kama inavyojulikana katika sheria za kimbunguni na sheria zisokuwa za kimbunguni. Bali ipo katika maumbile. Anaekanusha ni ambae maumbile yake yametofautiana na kanuni za kimaisha. Na hii ndiyo maana ambayo hadithi imeikusudia.

Yaani nimeamrisha kufikisha ulinganizi wa Mola wangu kwa hekima na mawaidha mazuri. Na mtu atakaponifanyia uadui na kupigana na mimi ili awakataze watu uhuru wao katika kuchagua imani basi nitapigana nae ili niwfanye watu huru kutokamana na anaewalazimisha kubaki katika ukafiri, ili iwe tunda la kuondoa kizuizi pamoja na ulinganizi kwa hekima na mawaidha mazuri ni washuhudie kuwa hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa ispokuwa Allah.

Na kwa kukusanya nukuu namna hii kunakoenda sambamba na kuwa na mtazamo kamili kwa Uislamu ndipo maana ya hadithi inakuwa wazi.

11- Muttafaqun 'alayh. Imepokewa na Bukhari (2942) (Kitabu cha Jihadi na Kutumwa Majeshi, Mlango wa Kulingania Mtume kwa Uislamu) na Muslim (2406) (Ubora wa Maswahaba, Mlango Katika Ubora wa Ali bin Abi Talib).

Ufupisho wa Utafiti

1- **Umuhimu wa Kiarabu** katika kufahamu nukuu za dini. Na hakuna njia ya kufikia makusudio ya maneno ispokuwa kwa lugha.

2- Umuhimu wa **kukusanya baina ya nukuu za sheria**, na mtazamo mkamilifu wa Uislamu, na kujua elimu zinazotumikia nukuu, kwa kurudi kwa wanazuoni waliokita katika ambalo dhahiri yake ni kuwa lina utata.

3- **Uislamu umeharamisha umwagaji damu na umeutilia mkazo na ugumu**, na umebainisha hukmu yake kwa nukuu za wazi. Allah amesema: {Anayeuba mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote} [Al-Maidah:32]. Na hilo lilidhihiri waziwazi katika miamala ya Mtume (rehema na amani zimshukie) na maswahaba zake watukufu (Mungu awaridhie).

4- Katika nukuu ambazo baadhi wamezitumia, na baadhi wamezifahamu vibaya ni hadithi hii nayo ni kinyume na madai yao.

5- Neno "uqaatil" katika hadithi ni tamshi la kutendeana ambalo kunahitaji kupatikane pande mbili ili litokee kwa maana **anampiga vita anaempiga na anaemuanzia uadui** na aliyemkataza kwa vita kutokamana na kufikisha Da'awa.

6- Neno la 'watu (al-Naas)', ji ni ya kujulikana. Yaani inawaongelea watu fulani nao ni waarabu washirikina ambao wamempiga vita mwenye kulingania na wakawa ni kizuizi kwake.

7- Haifai kumuua ambae amekataa kuingia katika dini. Allah amesema: {Hapana kulazimisha katika Dini.} [Al-Baqara:256]

8- **Kukubali dhahiri ya kila ambae amekubali Tawhid**, na hisabu yao ni kwa Allah kwa kumuachia Allah undani wao. Na kwahilo inafahamika uharamu wa damu zao, mali yao na cheo chao.

Kwahio hii hadithi **kwa hali yoyote haimaanishi kuuwa watu** au kuwaudhi au kuwalazimisha wala hailinganii kwa hilo kama tulivyobainisha.

MSURURU WA KUBADILISHA NA KUPOTOSHA NA KUZUSHA

Amesema Mtume (Rehema na Amani zimshukie na jamaa zake), "Wataibeba hii elimu kwa kila watu waadalifu wake na watauweka mbali upotevu wenye kuvuka mipaka na uzushi wa watu wenye kuleta batili na bayana za wajinga."¹²

Wamefahamu baadhi ya watu wenye fikra potevu na fahamu mbaya maneno ya Mwenyezi Mungu na maneno ya Mtume Wake kwa namna isiyo ambatana na mfumo wa kielemu iliyordhiwa kutoka kwa salaf (wema waliotangulia) wala haziambatani na makusudio na misingi mikubwa ya wahyi (ufunuo) wa kimola.

Walikusudia baadhi za aya za Quran Tukufu ambazo zilishuka juu ya wasiokuwa waisilamu wakazishukisha kwa waisilamu na wakachukuwa aya zilizokua kwa njia ya kuvuwa wakazifanya miongini mwazo hukumu yenze kuenea wakageuza na kupendua maana ya meneno ya Mwenyezi Mungu na hadithi za Mtume Wake Mtukufu kwa namna iliyopelekwa katika kuthibitisha au kuuandika fahamu iliyomakosa vibaya katika akili ya baadhi ya waisilamu walio wajinga iliyofanya kutoa ntja ya tabia na vitendo visivyokuwa na mafungamani na dini ya Kiislamu isiyokuwa na urongo.

Tunaweza kutambua katika madhumuni ya msururu juu ya ambao kwamba walitoka ndani yake watu wenye hizi fikra za makosa kuto kamana na kubadilisha au kupotosha kwa maana ya maneno ya Mwenyezi Mungu na maneno ya Mtume Wake na kwa fahamu wa watu wema waliotangulia.

12- Hadithi tangufu ameisahihisha Ibn Abdul Bar. Imeipokea kutoka kwa Ahmad Bin Hanbal kuwa yeye amesema, "Ni hadithi sahihi."